1805/103
KISWAHILI
Machi/Aprili 2025
Muda: Saa 3

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# CRAFT CERTIFICATE IN SOCIAL WORK AND COMMUNITY DEVELOPMENT

## MODULE I

KISWAHILI

**Saa 3**

**MAAGIZO**

*Mtihani huu una sehemu TANO muhimu.*
*Jibu Maswali yote.*
*Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.*
*Majibu yote yaandikwe katika kijitabu cha majibu ulichopewa.*
*Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***Maswali yote ni lazima yajibiwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*© 2025 The Kenya National Examinations Council*

**Geuza ukurasa**

## SEHEMU A - UFAHAMU (alama 20)

1. *Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Miaka kumi na minne ya ugatuzi nchini Kenya imeshudia maendeleo kwa viwango tofauti katika magatuzi yote. Kaunti zote arubaini na saba zimepiga hatua. Kwa jumla, nchi haipo pale ilipokuwa kabla ya kuidhinishwa kwa katiba ya mwaka elfu mbili na kumi. Ingawa bado kuna mengi yanayostahili kufanywa, ni kweli kusema kwamba matunda ya ugatuzi yameonekana.

Miundomsingi imeimarishwa. Barabara zilizokuwepo zimekarabatiwa na nyingine mpya kuanzishwa. Barabara hizo ni pamoja na zile ambazo zinaweza kutumika katika majira yote. Maeneo yaliyosambaziwa nguvu za umeme yameongezeka. Kwa sasa, idadi ya wananchi wanaotumia aina hiyo ya nishati ni zaidi ya ilivyokuwa.

Sekta ya elimu nayo haijaachwa nyuma. Shule nyingi mpya zimejengwa na nyingine nyingi kuongeza madarasa mpya. Hali hiyo imeongeza marudufu idadi ya watoto wanaopata elimu ya msingi na hivyo kuelekea **kuafikia** malengo ya kimataifa na ruwaza ya mwaka elfu mbili na thelathini.

Kwa upande wa afya, vituo vya kutoa huduma sasa viko karibu na wananchi. Katika maeneo mengi, zahanati zimejengwa takriban katika kila kata. Jambo hilo limewahakikishia wananchi huduma bora za afya. Visa vya kina mama kujifungulia nyumbani vimepungua. Hali kadhalika, vifo kutokana na magonjwa yaliyo na tiba vimepungua.

Ugatuzi pia umeleta huduma za kiserikali karibu na wananchi. Huduma hizo ni pamoja na usajili wa watu, usajili wa mashamba, uidhinishaji wa ramani za mijengo na nyinginezo. Hali hiyo imeokoa muda ambao wananchi walikuwa wakiupoteza na hivyo kuimarisha maendeleo. Serikali za kaunti pia zimeimarisha viwango vyao vya ushuru. Zaidi ya hayo, nafasi za kazi zimeongezeka. Serikali za maeneo gatuzi huwaajiri maafisa mbalimbali ili kuweza kutoa huduma zinazostahili.

Licha ya ufanisi ambao umetokana na ugatuzi, mengi mabaya pia yameshuhudiwa. **Hakika, hakuna mchele usiokuwa na ndume**. Ufisadi umeongezeka marudufu. Visa vya utoaji hongo ili kupata ajiri au huduma muhimu vinaripotiwa kila uchao. Jambo hilo limewavunja moyo raia na kufanya maendeleo ya kaunti nyingi kudorora.

Kwingineko, kuna kucheleweshwa kwa migao ya fedha kutoka kwa hazina kuu. Wafanyikazi wa serikali za kaunti hukosa mishahara kwa miezi kadhaa. Huduma muhimu pia hukwamizwa. Isitoshe, kuna ukosefu wa sera madhubuti zinazoongoza maeneo gatuzi. Wakati mwingine kuna sera zinazokinzana na zile za serikali kuu. Kwa sababu hiyo, kumekuwa na mizozo ya mara kwa mara kuhusu kwa mfano, ukusanyaji wa ushuru, huduma za afya na hata elimu ya chekechea.

Kuna tetesi kuhusu mapendeleo katika miradi ya maendeleo inayoanzishwa na serikali za kaunti.

Wengine hudai kwamba magavana huyapuuza maeneo wanayodhani hayakuwapigia kura au hata kwa sababu tu za kikabila au kijamii. Vilevile, kaunti nyingi zimekosa mipango mwafaka kuhusu mistakabali yao ya baadaye.

Kuna haja ya kupiga msasa ugatuzi kwa nia ya kuziba mianya, iliyokwishaonekana na kuudhibiti ufanisi uliopatikana. Serikali kuu nayo inafaa kutekeleza wajibu wake wa kuyaunga mkono magatuzi kwa kutoa fedha zinazohitajika kikatiba kwa wakati ufaao. Ushirikiano kati ya serikali kuu na serikali za kaunti ni muhimu kwani zote huwahudumia wananchi wa taifa hili.

(a) Eleza chanzo cha ugatuzi nchini Kenya. (alama 2)

(b) Msimulizi anamaanisha nini anaposema kuwa matunda ya ugatuzi yameonekana? (alama 6)

(c) Methali, **hakuna mchele usiokuwa na ndume**, imetumiwa katika kifungu. Thibitisha ukweli wa methali hiyo kwa hoja **tano** ukirejelea kifungu. (alama 5)

(d) Kulingana na kifungu, eleza mambo **matatu** yanayoweza kufanikisha ugatuzi. (alama 3)

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu.

(i) matunda

(ii) kuafikia

(iii) sera

(iv) kupiga msasa

(alama 4)

## SEHEMU D - MSAMIATI (alama 20)

4. (a) Rai ni wazo. Rai pia ni ______________________________. (alama 1)

(b) Tofautisha maneno yafuatayo kimaana. (alama 2)

(i) chaka

(ii) shaka

(c) Mkeka maalum unaowekwa kwenye sakafu ni _____________ na jiko linalotumiwa kuokea mkate ni ___________________. (alama 2)

(d) Eleza malipo yafuatayo:

(i) arbuni (alama 2)

(ii) kiokozi (alama 2)

(e) Randa ni kwa seremala, kipimajoto ni kwa ____________________ na sepetu ni kwa ________________________________. (alama 2)

(f) (i) Fauzia ni mke wa mwana wa mzee Omari. Je mzee Omari atamwitaje Fauzia? (alama 1)

_______________________________________________________________

(ii) Wanaume wawili wameoa mabinti wa Bi. Sowela. Je, wanaume hawa wanaitanaje? (alama 1)

_______________________________________________________________

(g) Joli alipata mkopo kutoka kwenye benki akautumia kama ___________ wa kuanzisha biashara. Yeye hupata faida na kulipa serikali _____________ kulingana na sheria. (alama 2)

(h) Jaza jedwali kwa misimu mwafaka. (alama 2)

| | |
|---|---|
| Mvua nyingi | ______________ |
| Baridi kali | ______________ |

(i) Eleza shughuli inayoendelezwa na Wizara ya Mashauri ya Nchi za Kigeni. (alama 2)

(j) Kupiga mbizi ni kuogelea na kuwa macho ni? (alama 1)

**SEHEMU E - ISIMU JAMII NA MASUALA IBUKA** (alama 10)

5. (a) Watu wanapokutana, huwa wanatumia lugha kwa namna fulani kuwasiliana. Eleza mambo **matano** ambayo hutawala matumizi ya lugha katika jamii. (alama 5)

(b) Umeteuliwa kuwashauri vijana ambao wanakaribia kukamilisha masomo ya shule za upili. Eleza hoja **tano** utakazozingatia katika ushari wako. (alama 5)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**